

**K**itabu hiki cha *Ufafanuzi wa Biblia Katika Mazingira na Utamaduni wa Kiafrika* ni kitabu cha kipekee kuwahi kuchapishwa—kinahusu ufafanuzi wa Biblia katika juzuu moja lililotolewa kwa mara ya kwanza hapa Afrika na wanatheolojia Waafrika ili kuyakidhi mahitaji ya wachungaji wa Kiafrika, wanafunzi na viongozi wa kanisa. Kwa kufasiri na kuzingatia matumizi ya Biblia katika muktadha halisi ya utamaduni wa Kiafrika ulivyo sasa; kitabu hiki kinayaeleza Maandiko Matakatiifu vizuri sana na kwa undani kwa njia bora zinazoahiki bara la Afrika kwa umuhimu wake.

Kitabu hiki cha *Ufafanuzi wa Biblia Katika Mazingira na Utamaduni wa Kiafrika* kinatoa ufasiri wa sehemu kwa sehemu ambao unaambatana na muktadha wa Kiafrika unaoeleweka kwa urahisi. Isitoshe, kitabu hiki kina bei nafuu na hivyo basi kukifanya kuwa mwongozo bora sana wa kuboma Biblia yote! Wasomaji kote duniam watafaidi na kuifurahia mitazamo mipya watakapopata hapa pamoja na jinsi mtindo wake wa moja kwa moja utakavyowahusisha kimoyo na kifikiria.

#### SIFA KUU

- Kimeandikwa na wasomi wa Biblia wa Kiafrika, katika Afrika, kwa Waafrika na ulimwengu wote.
- Kina ufafanuzi unaotoa ufasiri wa Maandiko Matakatiifu sehemu kwa sehemu pamoja na matumizi yake maishani.
- Kina zaidi ya makala nyeti 70 yanayoshughulikia masuala muhimu juu ya huduma barani Afrika sasa, na yaliyo na umuhimu kote duniani.
- Kimeandikwa na waandishi 70 wa Kiafrika wanaotoka katika maeneo yanayosema Kiingereza na yanayosema Kifaransa.
- Kinaupiku muktadha wa Kiafrika vizuri sana kwa jinsi kinavyoaeleza Maandiko Matakatiifu pamoja na imani ya Kikristo kwa wasomaji kote duniani.

#### MHARIRI MKUU

DR. TOKUNBOH ADEYEMO ndiye Msimamizi Mkuu wa Centre for Biblical Transformation. Hapo awali alikuwa Katibu Mkuu wa Association of Evangelicals in Africa. Ana shahada ya Uzamifu (PhD) kutoka Dallas Theological Seminary.

Msingi wa maisha ya Kikristo ni katika kulifahamu kwa usahihi Neno la Mungu.

Kanisa la Afrika linakua kwa haraka sana kuliko sehemu nyingine yoyote ulimwenguni. Lakini, linakosa kitabu chenye mafafanuzi katika lugha ambayo wengi wanaielewa. Upatikanaji wa kitabu hiki cha *Ufafanuzi wa Biblia Afrika Katika Mazingira na Utamaduni wa Kiafrika* ni hatua muhimu sana ya kihistoria kwa Kanisa la Afrika Mashariki, na mahali pengine popote kinapozungumzwa Kiswahili.

Augustino S.L. Ramadhani  
Jaji Mkuu wa Tanzania

Kwa muda mrefu Wakristo wanaotumia lugha ya Kiswahili wamekuwa wakisubiri kitabu cha aina hii. Lengo la kitabu hiki ni kumsaidia msomaji kuyaelewa Maandiko Matakatiifu yaani Biblia kwa kina zaidi na kwa mtazamo wa mazingira na utamaduni wa Kiafrika. Mifano iliyotumika kuelezea Biblia imetolewa kwa tamaduni mbalimbali za hapa Afrika. Hiki ni kitabu cha kwanza cha aina yake kilichoandikwa na wataalam wa Kiafrika na katika lugha ya Kiafrika. Kimeandaliwa kwa utalamu mkubwa na kwa kina cha mawazo.

— Rev. Canon Dr. Mkunga H.P. Mtingele  
Katibu Mkuu – Chama cha Biblia cha Tanzania

‘Juzuu hili la kipekee ni ishara kuu ya kukua kwa Ukristo barani Afrika. Popote pale Biblia inapendwa na kusomwa, kitabu hiki kitawasaidia watu kuelewa na vile vile kuishi kulingana na Maandiko Matakatiifu.

—Dkt. Christopher J.H. Wright,  
Mkurugenzi wa Kimataifa,  
Langham Partnership International



ISBN-10: 9966 805 12 5  
ISBN-13: 978 9966 805 12 6

# UFAFANUZI wa BIBLIA katika MAZINGIRA NA UTAMADUNI WA KIAFRIKA

*Juzuu Moja la Ufafanuzi  
Kimeandikwa na wasomi 70 wa Afrika*

**KIELELEZO**  
*Barua Ya Yakobo*

TOKUNBOH ADEYEMO  
*Mhariri Mkuu*

DIBAJI ZIMEANDIKWA NA JOHN R. STOTT NA ROBERT K. ABOAGYE-MENSAH